# SABATO TATU

**Sabato Ya Bwana**
**Sabato ya Wayahudi**
**Sabato ya Papa**

**E. J. WAGGONER**

# SABATO TATU

**Sabato ya Bwana**
**Sabato ya Wayahudi**
**Sabato ya Papa**

Na E. J. Waggoner

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Three Sabbaths (Apples of Gold Library No. 58) - Kiswahili

# SABATO TATU

**Sabato ya Bwana**
**Sabato ya Wayahudi**
**Sabato ya Papa**

---

Kwa kweli mtu anaweza kuongea juu ya Sabato katika uwingi wake kama vile mtu anavyoweza kuongea juu ya miungu mingi. “Hakuna Mungu ila mmoja tu. Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi; lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake VITU VYOTE VIMEKUWAPO, NA SISI KWA YEYE HUYO.” 1 Wakorintho 4:4-6. Kwa hiyo, ingawa kuna Sabato kadhaa, kama zinavyoitwa na watu, IKO MOJA TU AMBAYO NDIYO SABATO YA KWELI, yaani, SABATO YA BWANA.

## SABATO YA BWANA

Neno hili “Sabato” maana yake ni PUMZIKO/KUPUMZIKA … Ni neno la Kiebrania ambalo limehamishiwa katika lugha ya Kiingereza [na Kiswahili]. Waebrania walipolitumia neno hili “Sabato” lilikua na wazo lile lile kwako kama nano “kupumzika” lilivyo kwetu sisi. Kwa hiyo, ile amri ya nne kwetu inasema hivi hasa: “Ikumbuke siku ya KUPUMZIKA uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini SIKU YA SABA NI SIKU YA KUPUMZIKA YA BWANA [YEHOVA], Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, AKASTAREHE [AKAPUMZIKA] siku ya saba; kwa hiyo BWANA AKAIBARIKIA siku ya Sabato AKAITAKASA.” [Kutoka 20:8-11.]

Yatupasa sisi tusifanye kosa la kutoa hitimisho juu ya pumziko hilo la Bwana kwa kuangalia kile ambacho wanadamu wamezoea kukiita pumziko. Mungu si mwanadamu. Sisi ni afadhali tungejifunza kutoka katika pumziko la Mungu na kujua ni kitu gani hasa. Pumziko la Mungu sio tu pumziko la kimwili kutokana na uchovu. Jambo hilo tunalijua kutokana na mambo mawili ya kweli: Kwanza, “Mungu ni Roho.” Yohana 4:24. Sio “roho’ mojawapo kana kwamba alikuwa mmoja miongoni mwa wengi; lakini yeye ni Roho, kama ilivyoelezwa katika pambizo [fungu la pembeni mwa ukurasa] la Toleo lile Lililosahihishwa (Revised Version). Pili, “Mungu wa milele, BWANA, Muumba miisho ya dunia, HAZIMII, wala HACHOKI.” Isaya 40:28. Kwa hiyo, Bwana hakupumzika kwa sababu alikuwa amechoka, na PUMZIKO LAKE SI LA KIMWILI, BALI NI LA KIROHO, kwa kuwa yeye ni Roho. “Nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.”

Mungu alipumzika, si kwa sababu alikuwa amechoka sana, bali kwa sababu KAZI YAKE ILIKUWA IMEKWISHA. Kazi inapokwisha, na kufanywa vizuri, basi, hakuna kinachobaki isipokuwa kupumzika tu. Katika muda wa siku sita Mungu alimaliza kazi yake, naye alipoikagua, alitangaza kwamba ilikuwa “[NJ]EMA SANA.” [Mwanzo 1:31.] Hapakuwa na waa lo lote katika kazi ile. Ilikuwa haina dosari yo yote mbele zake. Basi, kwa kuwa kazi ile ya Mungu ilikuwa imefanyika na kufanyika vizuri sana mwisho wa siku ile ya sita, “AKASTAREHE [AKAPUMZIKA] SIKU YA SABA, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.” [Mwanzo 2:1-3.] Hakuwa na

mawazo yo yote yaliyomhuzunisha kuhusu kazi ile, wala masikitiko yo yote. Pumziko lake, kama mara kwa mara lilivyo pumziko liitwalo hivyo na wanadamu, halikuathiriwa na mawazo kama haya, "Kesho sina budi kwenda kufanya kazi ile tena;" wala na mawazo haya, "Natamani ningekuwa nimefanya sehemu hii ya kazi kwa njia tofauti kidogo;" wala na mawazo haya, "Laiti kama ningaliweza kuifanya kazi ile tena, ningefanya marekebisho mazuri;" wala na mawazo haya, "Kazi ya siku ile iliyopita ni mbaya sana hata siwezi kustahimili kuiangalia; nilikuwa nimechoka sana nilipoianza hata sikuweza kufanya nusu yake." Kwake hakuna kitu kama hicho. Kila sehemu ya kazi yake, hata uumbaji ule wa mwanadamu, ilikuwa kamilifu kadiri ilivyowezekana kuifanya hivyo, na Mungu alifurahi sana kutafakari juu ya kazi yake ambayo kutokana nayo alikuwa anapumzika, kwa sababu ilikuwa imemalizika na kuwa kamilifu.

Hilo ndilo pumziko analotupa sisi. Si jambo fulani analotutwika kwa lazima, bali ni jambo analotupa sisi kwa upendo wake na fadhili zake za milele. Kupumzika sio kazi ngumu ya kuchosha anayopewa mtu fulani. Si mzigo. Wale wanaoiangalia Sabato kama mzigo, hawajui Sabato ya Bwana ni kitu gani hasa. [Isaya 58:13,14.] Ni pumziko, pumziko kamilifu na safi.

Yesu Kristo ndiye yule Mmoja ALIYEYAUMBA MALIMWENGU YOTE, "kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi" [Kol. 1:16; Yn. 1:1-3,10,14], kwa hiyo, yeye Ndiye anayetupa PUMZIKO hili [SABATO – Mk. 2:27,28]. Kwa sauti kubwa anasema hivi kwa kila mtu, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami NITAWAPUMZISHA." Mathayo 11:28. PUMZIKO HILO LINAPATIKANA NDANI YAKE, kwa sababu ndani yake KAZI ZOTE ZA MUNGU ZIMETIMILIKA. Ndani yake ni UUMBAJI MPYA, na kama mtu ye yote akiwa ndani yake, basi, amekuwa KIUMBE KIPYA [2 Kor. 5:17; Efe. 2:8-10]. Pale msalabani Yesu alipiga kelele, alisema, "IMEKWISHA," akionyesha hivyo ya kwamba KATIKA ULE MSALABA WAKE TUNALIPATA PUMZIKO HILO KAMILIFU ambalo hupatikana tu kutokana na ile KAZI YA BWANA WETU ILIYOKWISHA.

Pumziko hilo hupatikana kwa IMANI. "Maana sisi TULIOAMINI tunaingia katika RAHA ile" [ = PUMZIKO = SABATO = STAREHE – Mt. 11:28,29; Mwa. 2:2; Kut. 31:17]. [Waebrania 4:3.] Kwa vipi? - Kwa sababu kwa imani tunayo kama yetu wenyewe kazi ile ya Bwana wetu iliyokwisha ambayo ni kamilifu. "Hii ndiyo kazi ya Mungu, MMWAMINI yeye aliyetumwa na yeye." Yohana 6:29. Kwa kumwamini yeye tunalipata pumziko hilo.

Pumziko analotupa Yesu ni pumziko tunalopata baada ya kuachana na dhambi zetu [uvunjaji wetu wa Amri Kumi – 1 Yoh. 3:4, AJKK]. Wale waliolemewa na mizigo mizito anaowaita kwenda kwake ni wale waliolemewa na MIZIGO MIZITO YA DHAMBI ZAO [UVUNJAJI WAO WA AMRI KUMI]. Wanadamu wote wamelemewa hivyo "kwa maana WOTE WAMEFANYA DHAMBI [WAMEVUNJA AMRI KUMI]" (Warumi 3:23). Matendo yetu [kazi zetu] bora sana ni bure kabisa (Isa. 64:6; Rum. 3:10-18]. Kristo atakuwa na watu [hapa duniani] walio na "juhudi katika MATENDO MEMA" (Tito 2:14,15); lakini matendo hayo mema ni lazima yawe ni yale ambayo Mungu mwenyewe ametenda kwa ajili yetu ndani ya Kristo. Ni kazi [matendo] yake tu inayodumu. "Kazi yake ni heshima na adhama, na haki yake yakaa milele." Zaburi 111:3. Kwa hiyo, "MMEOKOLEWA KWA NEEMA, KWA NJIA YA IMANI; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, NI KIPAWA CHA [ZAWADI YA] MUNGU; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Maana TU KAZI YAKE, tuliumbwa [upya] katika Kristo Yesu, TUTENDE MATENDO MEMA, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili TUENENDE NAYO." Waefeso 2:8-10. Wala "si kwa sababu ya matendo yetu ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa KUZALIWA KWA PILI NA KUFANYWA UPYA NA ROHO MTAKATIFU; ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu." Tito 3:5,6. Kwa hiyo, ni kwa kazi zake Mungu sisi tunaokolewa, wala si kwa kazi zetu wenyewe. Matendo mema yapo tele, tena yapo kwa ajili yetu

pia, lakini bila ya sisi kufanya kazi yetu yo yote, kwa njia pekee ya kazi ile kamilifu ya Mungu aliyofanya ndani ya Yesu Kristo. Endapo kazi hizo [matendo hayo] zingekuwa ni zetu wenyewe, basi, PUMZIKO HILO LINGEKUWA NI LETU WENYEWE; lakini Mungu anatupa PUMZIKO [SABATO] *LAKE* [SABATO *YAKE*], sio pumziko letu [sabato yetu], kwa sababu kazi zake peke yake ndizo zinaweza kuleta pumziko [sabato] kamilifu. "Amefanya UKUMBUSHO wa matendo yake ya ajabu." Zaburi 111:4, au, kwa maana ile ya neno kwa neno, "Ameweka UKUMBUSHO wa matendo yake ya ajabu." UKUMBUSHO huo ni SIKU YA SABA [JUMAMOSI], yaani, siku ile aliyopumzika [aliyostarehe/aliyosabatika (!)] na kuacha kufanya kazi zake zote alizozifanya [Mwa. 2:2]. Siku ile AMEIBARIKI na KUITAKASA, yaani, AMEIFANYA TAKATIFU [Mwa. 2:3; Kut. 20:11; 31:14,15]. UTAKATIFU WAKE HAUWEZI KUONDOLEWA KAMWE KUTOKA KATIKA SIKU HIYO [YA JUMAMOSI], kwa maana "lo lote alitendalo Mungu, LITASIMAMA MILELE." Haidhuru mwanadamu afanye nini, au aiangalieje siku hiyo, utakatifu wake unabaki pale pale [Isa. 58:13,14].

"Basi, imesalia RAHA YA SABATO [PUMZIKO LA SABATO, La Siku ya Saba - sio la Siku ya Kwanza) kwa watu wa Mungu [Ebr. 4:9; Isa. 66:22,23];" na siku ya saba [Jumamosi], ambayo Mungu anaitangaza kuwa ni pumziko lake la milele [Kut. 31:16,17], ndiyo kwayo anatujulisha sisi ukamilifu wa pumziko lake, kwa sababu yeye anatutaka sisi katika siku hiyo kutafakari juu ya UUMBAJI WAKE MPYA ULIOKWISHA NA KUTIMILIKA ndani yake [2 Kor. 5:17]. Siku ya saba [Jumamosi] inamfunua kwetu yule Mungu wa milele, Muumbaji mwenye uweza asiyechoka kamwe, aliyetenda na kuwawekea mema mengi wale wanaomtegemea mbele ya wana wa wanadamu [wasiozaliwa mara ya pili – Mwa. 6:2]. "Jinsi zilivyo nyingi fadhili zako ulizowawekea wakuchao; ulizowatendea wakukimbiliao mbele ya wanadamu!" Zaburi 31:19. Siku hiyo ya saba [Jumamosi] inatukumbusha kwamba sisi "TUMETIMILIKA KATIKA YEYE aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka" [Kol. 2:10]. Inatuambia kwamba japokuwa sisi tumetenda dhambi [tumezivunja zile Amri Kumi], na kuleta laana juu ya uumbaji mkamilifu wa Mungu, MSALABA WA KRISTO, unaoichukua laana hiyo [Gal. 3:13], unaifanya kazi ile kamilifu ya Mungu kuwa mpya na kuidumisha, ili kwa njia ya huo msalaba, sisi tupate kusimama bila waa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu [Yuda 24], tukifanana kabisa na mtu yule wa kwanza aliyeumbwa akiwa mkamilifu. "Mungu ashukuriwe kwa sababu ya KIPAWA CHAKE, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo" [2 Kor. 9:15].

**SABATO YA WAYAHUDI**

Kuna kitu kinachosemekana kama "Sabato ya Kiyahudi," yaani, Sabato ya Wayahudi, lakini hiyo iko tofauti kabisa na Sabato ya Bwana. Watu wengi wanafikiri kwamba kama mtu anaitunza siku ya saba [Jumamosi], basi, huyo anaitunza Sabato ya Wayahudi; lakini jambo hilo halifuati hivyo kabisa. Hakuna mtu ye yote atakayekuwa anaitunza Sabato ya Wayahudi endapo yeye ataitunza Sabato hiyo "kama ilivyoamriwa" [Luka 23:56; Kut. 20:8-11]. Pana tofauti ile ile kati ya Sabato ya Wayahudi na Sabato ya Bwana kama iliyopo kati ya mwanadamu na Mungu. Hebu na tufafanue:

"Siku ya saba ni Sabato ya BWANA" [Kut. 20:10]; lakini sisi tumekwisha kuona kwamba pumziko la Bwana ni la kiroho, ambalo siku ya saba [Jumamosi] inafanya ukumbusho wake. Mtu anaweza kuacha kufanya kazi ya kimwili katika siku ile ya saba ya juma [Jumamosi], wala asiweze kuitakasa Sabato ya Bwana. Mtu akiacha kufanya kazi yake siku ile ya Ijumaa jioni jua linapozama, halafu akiacha kufanya kazi zote mpaka siku inayofuata wakati wa kuchwa jua [Jumamosi jioni], akifanya hivyo tu kama mtindo wake fulani wa ibada, tena, ili kwamba mwili wake upate kuwa katika hali njema zaidi kumwezesha kwenda kufanya kazi yake tena, au akiwa na wazo kwamba kwa kufanya hivyo, basi, yeye anatimiza wajibu wake, na kupata upendeleo toka kwa Mungu, HUKO SIKO

KUITUNZA SABATO YA BWANA. Kuitunza Sabato ya Bwana ni KUJIFURAHISHA KATIKA BWANA [Isa. 58:13,14]. Wale wasiojifurahisha wenyewe katika Bwana, hawaitunzi Sabato, licha ya wao kujizuia kufanya kazi siku hiyo.

HAIWEZEKANI KABISA KWA MTU YE YOTE ASIYEKUWA MKRISTO KUITUNZA SABATO YA BWANA; kwa kuwa, kama vile tulivyokwisha kuona, pumziko la Mungu linatokana na kazi yake kamilifu, ambayo inapatikana tu ndani ya Kristo. "Maana sisi TULIOAMINI tunaingia katika RAHA [PUMZIKO/STAREHE/SABATO] ile" [Ebr. 4:3]. Kwa hiyo, hakuna Myahudi ye yote, aitwaye hivyo [kwa kuzaliwa], yaani, yule anayetofautishwa na Myahudi anayemwamini Kristo, ambaye anaitunza Sabato ya Bwana, japokuwa anaonekana akipumzika siku ya saba ya juma [Jumamosi]. PUMZIKO ANALOPUMZIKA NI LAKE MWENYEWE, wala sio lile PUMZIKO LA BWANA.

Je, unaiona tofauti yake? Sabato ya Wayahudi inaangukia katika siku ile ile ya juma [Jumamosi] sawasawa na ile Sabato ya Bwana, lakini kwa vyo vyote vile hiyo siyo kitu kile kile kimoja. Inamwakilisha huyo mtu peke yake, na KAZI YAKE MWENYEWE. Badala ya kuwa ishara ya KUHESABIWA HAKI KWA NJIA YA IMANI [Rum. 3:21-26] katika ile KAZI ALIYOIFANYA BWANA, yenyewe inageuka na kuwa ishara ya KUJIHESABIA HAKI WENYEWE [Gal. 2:15,16; Flp. 3:9], kama vile inavyodokezwa katika swali ambalo Wayahudi walimwuliza Yesu, "Tufanyeje ili [SISI] TUPATE KUZITENDA kazi za Mungu? [Yn. 6:28.] Wao walizihesabu KAZI ZAO [MATENDO YAO] kuwa zinalingana kabisa na KAZI ZA MUNGU. Utii wao haukuwa ni ule unaotokana na imani, bali ulikuwa ni wa kimtindo tu. Bwana na atuokoe mbali na Sabato kama hiyo. Ni mbali kabisa na wazo la kwamba sisi tunaokolewa kwa kuitunza Sabato hiyo ya Bwana, kwa kuwa TAYARI TUMEKWISHA KUOKOLEWA mbali na matendo [kazi] yetu wenyewe, na kupewa matendo [kazi] kamili ya Bwana. "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA" [Kut. 20:10], lakini na tujihadhari tusije tukaifanya kuwa pumziko la kichekesho tu. Hebu na tuichukue kama ilivyo hasa: PUMZIKO LA BWANA.

## SABATO YA PAPA

Hii ni kitu tofauti kabisa na ile Sabato ya Wayahudi, tena ni tofauti mno na Sabato ya Bwana. Sabato ya Bwana ni kule kuzikubali KAZI ZILE ALIZOZIFANYA MUNGU, na KUPUMZIKA KATIKA KAZI HIZO PEKE YAKE [Ebr. 4:10,11], HUKU TUKIMRUHUSU KUFANYA KAZI NDANI YETU, kutaka kwetu na kutenda kwetu, ili kulitimiza kusudi lake jema [Wafilipi 2:12,13]; Sabato ile ya Wayahudi inawakilisha juhudi zile za bure kabisa za watu wale wenye bidii, na WANAOJITUMAINIA WENYEWE KUZIFANYA KAZI ZILE AMBAZO NI MUNGU MWENYEWE ANAYEZIFANYA, tena ambazo ni MUNGU PEKE YAKE AWEZAYE KUZIFANYA; lakini ile Sabato ya Papa inaashiria UWEKAJI WA KAZI YA MWANADAMU MAHALI PA KAZI YA MUNGU, na kuiona [hiyo kazi ya mwanadamu] kwamba sio tu nzuri, bali hata ni bora zaidi [ukilinganisha na ile ya Mungu]. Sabato hiyo hata inadiriki KUUTUPILIA MBALI KABISA MFUMO WA AMRI ILE YA [SABATO] YA BWANA [Kut. 20:8-11]. Hebu, basi, na tuone jinsi ilivyo Sabato hiyo.

Sabato ya Bwana imeongelewa vya kutosha mpaka sasa. Tunajua ni kitu gani. Tumekwisha kuona kwamba Sabato ya Wayahudi ni ile ya kushika *mfano tu* wa Sabato ya Bwana, bila kuwa na nguvu yake ya kuitunza, ambayo inaweza kupatikana tu kwa njia ya imani. Inaangukia katika siku ile ile [ya Jumamosi], lakini hiyo ni SABATO YA MWANADAMU, wala sio ya Bwana. Sabato ya Papa haina uhusiano wo wote na Sabato ya Bwana, hata katika mfumo wake, lakini INAIKATAA KATAKATA

SABATO YA BWANA. Hivi ndivyo kisemavyo kitabu kimoja cha Wakatoliki wa Roma, chenye kichwa hiki, "Njia ya Hakika ya Kuipata Dini ya Kweli":-

"Utunzaji [utakasaji] wa Jumapili NI JAMBO LA LAZIMA KABISA KWA WOKOVU; lakini maneno kama hayo hayajaandikwa mahali po pote katika Biblia; kinyume chake, Biblia inasema hivi, 'Ikumbuke Siku ya Sabato uitakase' (Kutoka 20:8), siku hiyo ni Jumamosi, wala sio Jumapili; kwa hiyo Biblia haina mambo yote yaliyo ya lazima kwa wokovu."

Huo ni mfano mmoja tu ulionukuliwa miongoni mwa madondoo mengi yanayofanana na hilo ambayo tungeweza kuyatoa hapa, lakini yatosha tu kuonyesha kwamba katika utunzaji wa Jumapili Kanisa Katoliki linalikataa katakata Neno la Bwana, tena LINAJIINUA JUU YA NENO HILO [ = KRISTO - Ufu. 19:13; Yn. 1:1-3; 14:21,23,24; 2 The. 2:3,4]. Limeiweka Sabato yake katika siku [ya Jumapili] iliyo tofauti kabisa na ile ya Sabato ya Bwana [Jumamosi], - SIKU AMBAYO HATA MUNGU MWENYEWE ASINGEWEZA KUIFANYA KUWA SABATO YAKE, KWA SABABU KATIKA SIKU HIYO NDIPO ALIPOANZA KAZI YAKE YA UUMBAJI [Mwanzo 1:1-5], - ili lipate kuyatilia mkazo madai yake na kuyaweka juu kuliko Mungu. Lingependa kuwafundisha watu ya kwamba ni lazima WALITII KANISA KULIKO MUNGU.

Zingatia kwamba dondoo tulilolinukuu linazungumzia juu ya umuhimu wa "kuitakasa Jumapili." Lakini MUNGU HAJAIFANYA JUMAPILI KUWA TAKATIFU. Kusema kweli, Biblia haina habari kabisa na siku kama hiyo [iitwayo Jumapili]. Inaijua tu SIKU YA KWANZA YA JUMA [yaani, Jumapili], ambayo inaiita kuwa ni SIKU YA KAZI [Kut. 20:9,10; Eze. 46:1], lakini siku hiyo ya Jumapili imewekwa ikiwa na sehemu za siku hizo mbili, ilibuniwa kule Roma. Siku peke yake ambayo Mungu amepata kuzungumzia habari zake kuwa ni TAKATIFU ni siku ile ya saba ya juma [yaani, Jumamosi]. Siku hiyo ni yeye mwenyewe aliyeifanya kuwa takatifu, na yote anayotutaka sisi kufanya ni KUITAKASA. Lakini kwa vile Mungu hajaifanya Jumapili kuwa takatifu, basi, inafuata kwamba kama mwanadamu anataka kuitunza siku hiyo kama siku takatifu, basi, NI LAZIMA MWANADAMU MWENYEWE AIFANYE IWE TAKATIFU. Utakatifu wote duniani ambao Jumapili inao ni ule ambao mwanadamu anaipa. Kwa hiyo, hiyo Sabato ya Jumapili inasimama kama ISHARA [DALILI/CHAPA] YA UWEZO AMBAO MWANADAMU HUYO ANAJIDAI KUWA ANAO ILI KUIFANYA IWE TAKATIFU. Kwa maana kama mwanadamu anao uwezo wa kukifanya kitu kimoja kuwa kitakatifu, basi, ni dhahiri kwamba anaweza kukifanya kitu cho chote kuwa kitakatifu. KAMA MWANADAMU HUYO ANAWEZA KUIFANYA NA KUITUNZA SIKU KAMA TAKATIFU, BASI, ANAWEZA KUJIFANYA NA KUJITUNZA MWENYEWE KAMA MTAKATIFU. Hivyo Sabato ya Papa ni ISHARA [CHAPA – Ufu. 13:16-18] YA MADAI YA PAPA ANAYOTOA KWAMBA YEYE ANACHUKUA MAHALI PA MUNGU KAMA MTAKASAJI WA WENYE DHAMBI.

Wakati ambapo siku ya saba ni ISHARA [DALILI/MUHURI] YA UWEZA WA MUNGU WA KUOKOA KUTOKANA NA KAZI ZAKE, Jumapili ni ishara ya mwanadamu kujitwalia madaraka ya kujiokoa mwenyewe kwa kazi zake [matendo yake] mwenyewe, kwa kujitenga kabisa na Bwana, na bila ya kumjali kabisa. Siku hiyo [ya Jumapili] INAMKATAA BWANA KWA KULIKATAA KATAKATA NENO LAKE. Zingatia kwamba maneno haya yanaongelea juu ya Jumapili ya Papa, wala sio juu ya wote wanaoiona siku hiyo kuwa ni takatifu. Wako maelfu kwa maelfu wanaoitunza siku hiyo ya papa, kuwa unyofu wa moyo wakidhani kwamba hiyo ndiyo Sabato ya Bwana. Naam, hao wanaamini katika kuhesabiwa haki kwa imani, ijapokuwa, bila ya wao kujua, wanaitunza ishara hiyo [ya Jumapili] inayowakilisha kuhesabiwa haki kwa matendo. Ni kwa faida ya hao ndiyo maana makala hii imeandikwa, ili wawe na msimamo mnyofu kabisa katika kuikiri imani yao. Hapa tunashughulika tu na mambo ya kweli, bila kujali wanadamu wanahusianaje nayo; na mambo hayo ya kweli ni kwamba Sabato ya Bwana [Jumamosi] inawakilisha kuhesabiwa haki kwa imani [Eze.

20:12,20; Kut. 31:13-17; Isa. 58:13,14; 56:1-8]; SABATO YA PAPA [JUMAPILI] MAANA YAKE NI KUHESABIWA HAKI KWA MATENDO, ni kutegemea matendo ya mwanadamu mwenyewe. Je! wewe utasimama upande gani [katika suala hili nyeti]?

---

**ANGALIA:** Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [ ] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza zaidi. Yasinukuliwe.